

Chanjo za COVID-19 – Valensi Moja na Valensi Mbili

**Vaccinate
WA**
CovidVaccineWA.org



Huenda umesikia istilahi "valensi moja" au "valensi mbili" zikitumika kuelezea chanjo za COVID-19. Hebu tuongee kuhusu tofauti kati ya aina hizi mbili za chanjo, na umuhimu wa kupokea busta ya valensi mbili iliyosasishtwa wakati unastahiki kupata.

Kuna tofauti gani kati ya chanjo zenye valensi moja na valensi mbili?

Chanjo ya valensi moja ni chanjo yenye utungo mmoja au viambajengo vya virusi.

Chanjo ya valensi mbili ni chanjo yenye tungo mbili au viambajengo vya virusi.

Ni chanjo gani za COVID-19 ni za valensi moja, na zipi ni za valensi mbili?

Chanjo asili za COVID-19 za misururu yote ya msingi na busta asili ni za valensi moja*. Chanjo hizi ziliundwa kutoka kwenye utungo asili wa virusi ambavyo huwa vinasababisha maradhi ya COVID-19.

Busta za COVID-19 za Pfizer na Moderna zilizosasishtwa ni zenye valensi mbili. Ziliundwa kwa utungo asili wa COVID-19, na tungo za aina mpya ya omicron, BA.4 na BA.5.

Je, chanj zenye valensi mbili zinafanya kazi zaidi ya chanjo yenye valensi moja?

Majaribio ya tiba za awali ya busta zilizosasishtwa zimeonyesha kuwa chanjo za COVID-19 zenye valensi mbili hutoa ulinzi mkubwa dhidi ya ugonjwa wa COVID-19 ikilinganishwa na busta za valensi moja na inaweza kuzidisha kipindi cha ulinzi dhidi ya maradhi makali au kifo, hasa kutoka kwa aina ya omicron.

Busta ya Novavax ni ya valensi moja na inapatikana kwa watu wazima waliokamilisha misururu ya msingi ya chanjo lakini awali hawakuwa wamepokea busta ya COVID-19 -- na iwapo hawawezi au hawatapokea busta ya valensi mbili ya mRNA iliyosasishtwa. Busta za Novavax **hazilengi tungo za aina ya omicron.*

Kwa nini ni muhimu kupata busta ya valensi mbili?

Ni muhimu kupata busta yenye valensi mbili kwa sababu ndiyo aina pekee ya chanjo ya COVID-19 ambayo iliundwa ili kulinda watu dhidi ya tungo hatari zaidi za omicron za COVID-19 ambazo kwa sasa zinasambaa Marekani.

Je, nafaa kupata busta yenye valensi mbili iwapo tayari nimepokea COVID-19 au nilipokea busta yenye valensi moja hapo awali?

Ndiyo, inapendekezwa kuwa upate busta yenye valensi mbili iliyosasishtwa iwapo unastahiki licha ya kuambukizwa COVID-19 awali au kabla ya busta yenye valensi moja. Kwa ufaafu kamili, watu ambao hivi karibuni waliambukizwa COVID-19 wanaweza kuzingatia kuchelewesha chanjo yoyote ya COVID-19, ikiwa pamoja na dozi ya busta iliyosasishtwa, kuanzia miezi 3 kuanzia wakati ambapo dalili zao zilianza au wakati ambapo walipimwa wakapatikana na maambukizo.

Je, nahitaji kupokea chapa maalum ya busta yangu yenye valensi mbili?

Watoto walio na umri wa miaka 6 hadi miaka 4 wanafaa kupokea busta ya valensi mbili iliyosasishtwa ambayo ni sawa na chapa ya chanjo waliyopokea misururu ya msingi.

Watoto walio na umri wa miaka 5 waliokamilisha misururu ya msingi ya Pfizer wanaweza kupokea busta ya valensi mbili iliyosasishtwa ya Pfizer pekee.

Watoto walio na umri wa miaka 5 waliokamilisha misururu ya msingi ya Moderna au Pfizer wanaweza kupokea busta ya valensi mbili iliyosasishtwa ya Moderna au Pfizer.

Watu walio na umri wa miaka 6 na zaidi wanaweza kupokea busta yenye valensi mbili ya Moderna au Pfizer licha ya chapa waliyopokea katika misururu yao ya msingi.